

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,

MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kama mnavyofahamu Siku ya utumishi wa umma huadhimishwa na kila nchi Barani Afrika kila tarehe 23 Juni ya kila mwaka kwa lengo la kuthamini kazi zinazofanywa na sekta ya utumishi wa umma katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Tanzania itakuwa mwenyeji wa sherehe za maadhimisho ya Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika. Sherehe hizi zitafanyika jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 15 hadi 19 Juni 2009.

Kauli mbiu ya maadhimisho ya siku ya utumishi wa umma kwa mwaka huu ni: ***Kuimarisha Ushirikiano Thabiti Baina Ya Serikali na Wadau katika Utoaji Huduma na Kuleta Maendeleo Endelevu Afrika.***

Kama sehemu ya maadhimisho hayo pia yatafanyika mambo yafuatayo:

✚ Mkutano wa Mawaziri wa Utumishi wa umma Barani Afrika kuanzia tarehe 17 hadi 18 Juni 2009 katika Hoteli ya Kilimanjaro Kempiski, Dar es Salaam. Mkutano huu umelenga kujadili kwa kina masuala yanayojitokeza katika kusimamia utumishi wa umma na kuangalia namna ya kuboresha utumishi wa umma kutokana na changamoto zilizopo. Mkutano huo utafunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Ali Mohamedi Shein.

✚ Maonesho ya wiki moja ya kazi mbalimbali zinazofanywa na Taasisi za Serikali. Maonesho hayo yatakayoshirikisha zaidi ya Taasisi 160 za Serikali hapa nchini pamoja na Taasisi kutoka baadhi ya nchi za Afrika yatafanyika kuanzia tarehe 15, Juni 2009 kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam. Maonesho ya mwaka huu yatafunguliwa rasmi tarehe 16 Juni 2009 na Rais wa Zanzibar Mhe. Dkt. Aman Abeid Karume.

✚ Sherehe za siku ya Utumishi wa Umma Afrika zitafikia kilele chake tarehe 19 Juni 2009 ambapo Mgeni Rasmi katika sherehe hizo atakuwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete. Baada ya tarehe hii ya kilele kwa ngazi ya Bara la Afrika, maonesho ya wiki ya utumishi wa umma kwa Taasisi za Serikali ya Tanzania yataendelea hadi tarehe 23 Juni 2009.

🇹🇿 Sambamba na maadhimisho ya Kimataifa, Tanzania itaendelea kuadhimisha Siku ya Utumishi wa Umma kwa kupitia maonesho ya Taasisi za Serikali hadi Tarehe 23, Juni, 2009 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Uamuzi wa kuwa na siku ya Utumishi wa Umma Afrika ulifikiwa na Mawaziri wa Utumishi wa Umma wa nchi za Afrika waliokutana Windhoek Namibia mwaka 2001. Pia siku hiyo imekuwa inaadhimishwa katika ngazi ya Kibara katika mmojawapo ya nchi za Afrika mara moja kwa miaka miwili. Mara ya mwisho sherehe za aina hii zilifanyika Windhoek, Namibia.

Wananchi mnaombwa kufika kwa wingi kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam kuanzia tarehe 15 hadi 23 Juni 2009 ili kutoa kero kuhusu huduma zinazotolewa na vyombo mbalimbali vya Serikali, kupata huduma kutoka kwa baadhi ya taasisi na kuelimishwa kuhusu huduma mpya na zile ambazo zimeboreshwa na Serikali.

Imetolewa Na:

Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma,

Dar es Salaam,

Barua pepe: permsec@estabs.go.tz

Tovuti: www.estabs.go.tz

Tarehe 5 Juni 2009